Kanuni za Barabara

Highway Code-Inside-Swa.indd i 9/25/08 3:14:36 PM

©Wizara ya Miundombinu
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Oktoba 2008

ISBN 978 9987 9171 4 3

Highway Code-Inside-Swa.indd ii 9/25/08 3:14:38 PM

Contents

Dibaji....1
Utangulizi....3
Ushauri kwa watumiaji wote wa barabara....5
Sheria za watembea kwa miguu....6
- Mwongozo wa jumla....6
- Kuvuka barabara....7

Sheria za waendesha baiskeli....9
- Mwongozo wa jumla....9
- Makutano ya barabara....12
- Kuvuka barabara....13

Sheria za abiria anayetumia mabasi, daladala, teksi na pikipiki....14
Sheria za watu wanaochunga wanyama....15
Sheria za madereva wa magari....16
- Kabla ya kuendesha....16
- Wakati wa kuendesha....19
- Mwendo....23
- Kulipita gari jingine....25
- Makutano....29
- Ushauri maalumu kwa madereva kwenye sehemu zenye mzunguko....34
- Uendeshaji wa usiku au kwenye hali mbaya ya hewa....35
- Kurudi nyuma....37
- Kuegesha....38
- Kuwajali watembea kwa miguu na watumiaji wengine wa barabara wanaoweza kuathirika....39
- Panapokatisha Reli....41

Kuharibika....43
Iwapo kuna ajali....44
Huduma ya Kwanza....45
Alama za barabarani....49

Highway Code-Inside-Swa.indd iii 9/25/08 3:14:38 PM

Highway Code-Inside-Swa.indd iv 9/25/08 3:14:38 PM

Dibaji

Kanuni za Barabara ni jumla ya sheria na ushauri wa namna ya kutumia barabara zetu. Kanuni hizi zinahusisha sheria ya barabarani na desturi ya uendeshaji mzuri. Migogoro ni kawaida kwenye mfumo wowote wa barabara, lakini iwapo wote tutafuata kanuni zilezile tunapokuwa barabarani, na kutenda katika namna ya kujali na kuwajibika kwa wengine, usafiri wetu barabarani utakuwa wa salama na usio wa mashaka. Kanuni za Barabara zitawafaa hasa madereva wanafunzi, kwani wanahitaji kuzifahamu ili kufaulu mafunzo yao ya udereva, lakini tunashauri kuwa, hata kama umekuwa ukiendesha gari kwa muda fulani, soma Kanuni hizi ili kujikumbusha maarifa yako kuhusu sheria. Pia Kanuni za Barabara zinajumuisha ushauri unaofaa kwa watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na watumiaji wengine wa barabara wanaoweza kudhurika – pia wao wana wajibu wa kuendesha katika namna ya kujali na umakini.

Tunawaomba watumiaji wote wa barabara kujifunza Kanuni za Barabara na kufuata ushauri uliotolewa. Iwapo kila mmoja atafanya hivi, usafiri wa barabarani utakuwa wa salama na wa kufurahisha zaidi.



Mheshimiwa Lawrence Masha
Waziri wa Mambo ya Ndani



Mheshimiwa Shukuru Kawambwa
Waziri wa Miundombinu

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:1 9/25/08 3:14:38 PM

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:2 9/25/08 3:14:39 PM

Utangulizi

Sheria ya Barabarani [Kifungu cha 168 R.E. ya 2002] imetunga Sheria za Barabara kama mwongozo rasmi wa namna ya kutumia barabara zetu kiusalama na kwa ubora. Ni kwa ajili ya wale wote wanaosafiri barabarani, ikiwa ni pamoja na watembea kwa miguu,waendesha baiskeli, waendesha pikipiki, na madereva. Iwapo kila mmoja atafuata sheria hizi kutakuwa na matukio machache ya kugongana na foleni.

Kanuni za Barabara ni mchanganyiko wa sheria na Ushauri. Kanuni hizi ni tafsiri rahisi ya maelezo magumu ya Sheria za Barabarani na kanuni zinazohusiana nazo. Iwapo hutazifuata unavunja sheria, na kama utakamatwa na kutiwa hatiani utatozwa faini na kuzuwiwa kuendesha. Unaweza pia kupelekwa jela kwa miaka hadi mitano. Unapoona neno "LAZIMA" au "SI LAZIMA" maana yake ni kuwa kisheria unapaswa kufuata maelekezo haya. Sheria za barabarani zitabadilika katika miaka ijayo na hunabudi kuwasiliana na Kituo cha karibu cha polisi iwapo una shaka kuhusu kanuni za sasa.

Kanuni za Barabara zinajumuisha ushauri mzuri kwa watumiaji wa barabara. Kushindwa kufuata ushauri huu peke yake si kosa, lakini kunaweza kutumika kortini kama ushahidi kuwa ulikuwa ukienda kwa namna isiyo salama.

Kuendesha kwenye barabara zetu zenye watumiaji wengi ni kazi ngumu na si rahisi kufuata kanuni na ushauri unaoongoza kila hali inayoweza kutokea. Tumia maarifa ya kawaida, na mara zote waruhusu wengine kupita iwapo itasaidia kuepuka ajali.

Sheria za Barabara zinajaribu kueleza vitu kwa lugha rahisi, lakini baadhi ya istilahi zilizotumika zinaweza kuwa ngeni kwako, au zenye maana tofauti kidogo na ile unayoifahamu. Mwongozo mfupi umetolewa hapo chini:
"Dereva" maana yake ni mtu yeyote anayeendesha gari au vitu vingine (pamoja na baiskeli) au anayeongoza wanyama barabarani.
"Njia mbili" maana yake ni barabara ambayo barabara zinazokwenda upande tofauti zinatenganishwa kati au na kizuizi.
"Kuruhusu wengine" maana yake ni kuwa dereva asiendelee, iwapo kufanya hivyo kutawalazimisha madereva wa magari mengine kubadili mwendo au mwelekeo kwa haraka.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:3 9/25/08 3:14:39 PM

“Njia” maana yake ni kipande cha barabara ambacho kimeonyeshwa kwa matumizi ya magari yanayokwenda kwa mstari mmoja.
“Mtumiaji wa barabara” maana yake mtu yeyote anayesafiri, au aliyepo barabarani, au kwenye gari barabarani.
“Magari barabarani” maana yake magari yanayokwenda.
“Gari” maana yake mashine yoyote inayoendeshwa barabarani kwa nishati yoyote na ikijumuisha baiskeli, mikokoteni ya kusukumwa kwa mikono na mikokoteni ya kuvutwa na wanyama.
“Alama za pundamilia” maana yake alama za kivuko cha watembea kwa miguu inayoonyeshwa na mistari miyeupe sambamba na mwelekeo wa barabara.

Kanuni hizi za barabara zimetolewa na Kitengo cha Usalama Barabarani cha Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi. Kazi hii ilisaidiwa na Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Denmark. Vyanzo vingi vilipitiwa ili kupata ushauri mzuri wa kutumia barabara kiusalama. Waandishi wanapenda kushukuru kwa kutumia maarifa ya Mwongozo wa SATCC kwa Madereva Wanafunzi, Sheria za Barabara za Uganda, na rasimu ya mwanzo ya Sheria za Barabara iliyotungwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Jumuia ya Msalaba Mwekundi Tanzaniakwa ukarimu walitusaidiakatika sehemu ya “Msaada wa Kwanza”.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:4 9/25/08 3:14:39 PM

Ushauri kwa watumiaji wote wa barabara

Uwe katika hali nzuri. Unatakiwa kuwa katika hali nzuri kuweza kuitumia barabara kwa usalama. Iwapo hutakuwa katika hali nzuri, usiendeshe. Tafuta msaada iwapo unatakiwa kwenda mahali fulani. Usitumie barabara iwapo unatumia pombe au dawa za kulevya kiasi cha kukufanya kutojiweza. Iwapo unatumia dawa muombe ushauri daktari wako kama unaweza kuendesha.

Wajibika. Una wajibu wa kufanya jitihada yoyote kuepuka kufanya kitu chochote kinachoweza kuleta madhara kwa wengine. Hivi hujumuisha vitu vinavyojulikana kuwa vya hatari, mfano kuendesha kwa kasi, kunywa pombe halafu ukaendesha, na kulipita gari jingine kwenye kona.

Kuwa makini. Utumiaji salama wa barabara unahitaji umakini wako mkubwa, kwa dereva au mtembea kwa miguu. Usiwaruhusu wengine wakuvuruge.

Kuwa mtulivu na mvumilivu. Epuka kuwa na hasira kuhusu tabia mbaya ya wengine. Usijaribu kuwaadhibu. Kuwa mvumilivu kwenye foleni, na usifanye fujo kwa kujaribu kuwapita walio mbele yako. Usitumie barabara iwapo una hasira, umesisimuliwa sana au kufadhaishwa sana na jambo fulani.

Wasaidie wengine. Iwapo kila mmoja atafuata sheria na kuwasaidia wengine kutapunguza kuchelewa. Ubinafsi huharibu mambo kwa kila mtu na inaweza kuwa hatari.

Walinde walio katika hatari. Una wajibu wa kuwalinda na kuwasaidia wazee, walemavu, na watoto. Madereva wa magari lazima wawe makini zaidi wanapochangia barabara na wale wenye uwezo mdogo wa kujikinga na majeruhi – hawa ni pamoja na watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na waendesha pikipiki.

Usipiga kelele zisizo na sababu. Kelele kupita kiasi huvuruga na kuchosha. Iwapo unaendesha gari kumbuka kuwa honi hutumika tu wakati wa dharura.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:5 9/25/08 3:14:39 PM

Sheria za watembea kwa miguu

Mwongozo wa jumla

Zingatia Wajibu. USIFANYE tabia yoyote inayoweza kuwa ya hatari kwako au watumiaji wengine wa barabara.

Tumia njia ya watembea kwa miguu. Iwapo kuna njia ya watembea kwa miguu itumie. Usitembee karibu na ukingo wa barabara mgongo wako ukiwa upande wa barabara. Usitembee barabarani isipokuwa unapokuwa umehakikisha kuwa ni salama kufanya hivyo.



Tembea upande wa kulia. Endapo kuna njia ya watembea kwa miguu, pita upande wa kulia wa barabara ili uweze kuyaona magari yanayokuja. Inapowezekana, hususan kwenye barabara nyembemba au kwenye mwanga mdogo, tembea kwenye mstari mmoja na wengine. Uwe mwangalifu sana kwenye kona kali za upande wa kulia.

Jiwezeshe kuonekana kwa urahisi. Vaa au beba kitu ambacho mara zote kitakusaidia kuonekana. Vitu vinavyong'aa au kuakisi mwanga vitakusaidia kuonekana kunapokuwa hakuna mwanga wa kutosha mchana. Wakati wa usiku tumia vitu vinavyoakisi vinavyoweza kuonekana katikamwanga.

Kutembea na watoto. Usimruhusu mtoto mdogo atembee peke yake kwenye njia ya watembea kwa miguu au barabarani. Unapotembea na watoto, tembea katikati yao na barabara ukiwa umeshika kwa nguvu mikono yao.

Kutembea kwenye kundi. Iwapo kundi la watu linashiriki kwenye matembezi yaliyopangwa barabarani, watembea upande wa kulia. Waandaaji wahakikishe kuna walinzi mbele na nyuma waliovaa nguo zinazong'aa katika mwanga wa mchana na nguo zinazoakisi wakati wa giza.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:6 9/25/08 3:14:40 PM

Kuvuka barabara

Fuata Kanuni hizi za Uvukaji:

1. ***Tafuta sehemu salama ya kuvuka***
2. ***Simama kwenye ukingo wa barabara***
3. ***Angalia magari barabarani kushoto, kulia na sehemu zote kukuzunguka, na sikiliza.***
4. ***Kama kuna gari linakuja liache lipite***
5. ***Wakati hakuna gari linalokuja, vuka moja kwa moja barabara-usikimbie***
6. ***Angalia na sikiliza magari wakati wa kuvuka***

Mahali salama pa kuvukia. Chagua sehemu unapoweza kuona pande zote, na ambapo dereva anaweza kukuona. Kwa sababu hii, vuka barabara vizuri mbali na kona kali yoyote. Mahali ambapo ni salama kuvuka barabara, ni pamoja na kwenye taa za barabarani, kwenye alama za pundamilia, kiplefti, madaraja ya waendea kwa miguu na njia za chini, au mahali alipo ofisa wa polisi, mwongoza kivuko cha shule au magari.

Kuvuka kwenye kizingwa. Iwapo kuna kizingwa katikati ya barabara, tumia Kanuni za Uvukaji kuvuka hadi kwenye **kizingwa** na kisha simama. Tumia utaratibu uleule kuvuka sehemu iliyobaki ya barabara.



Kuvuka kwenye alama za pundamilia. Iwapo kuna alama za pundamilia karibu zitumie. Mpe dereva muda wa kutosha kukuona na kusimama kabla ya kuvuka. Madereva wanatakiwa kisheria wasimame pindi unapoanza kuvuka kwenye alama, lakini usivuke hadi wanaposimama. Kisha vuka moja kwa moja, lakini endelea kuangalia na kusikiliza.



Kuvuka kwenye taa za barabarani. Katika baadhi ya sehemu kuna ishara za taa za barabarani zinazoyaongoza magari wakati wa kusimama na watembea kwa miguu wakati wa kuvuka. Wakati ishara ya mtu aliyewima mwenye rangi nyekundu inapoonyeshwa USIVUKE. Wakati taa zikibadilika kuonyesha ishara ya “mtu anayetembea” mwenye rangi ya kijani, angalia kuwa magari yamesimama na kisha vuka kwa uangalifu. Baada ya muda ishara ya rangi nyekundu, au wakati mwingine ishara ya rangi ya kijani, inawaka ghafla, na hii maana yake usianze kuvuka, kwa sababu magari karibu yataanza kwenda tena.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:7 9/25/08 3:14:40 PM

Iwapo taa za barabarani hazina ishara maalumu kwa watembea kwa miguu, angalia kwa makini na usivuke hadi taa nyekundu zikiwaka na magari kusimama. Pamoja na hayo, angalia magari yanayopinda kona. Kumbuka kuwa taa za barabarani zinaweza kuruhusu magari kutembea kwenye baadhi ya njia wakati njia nyingine zikiwa zimesimama.

Vivuko vinavyoongozwa na polisi, askari wanaoongoza magari na waongozaji wa shule. Iwapo kuna ofisa wa polisi au mtu mwingine mwenye mamlaka ya kuongoza magari, USIVUKE barabarani hadi wakuashirie kufanya hivyo. Mara zote vuka mbele yao.

Usipande juu ya uzio. Katika sehemu nyingine uzio umewekwa ili kuwazuia watembea kwa miguu kuvuka barabara na kuwaongoza mahali salama pa kuvukia. Usipande juu ya uzio, au kutembea katikati yake na barabara. Vuka kwenye nafasi iyowekwa.

Kuvuka mitaa ya barabara moja na njia ya basi na baiskeli. Angalia ni njia ipi ambayo magari yanakwenda, kisha tumia Kanuni za Uvukaji kuvuka barabara. Kuwa makini sana kwa sababu magari yanaweza kuwa yanakwenda kasi sana kuliko kawaida.

Usivuke katikati ya magari yaliyoegeshwa. Iwapo utalazimika kuvuka katikati ya magari, tumia ukingo wa nje wa magari iwapo barabara ina ukingo. Simama hapo na hakikisha kuwa unaweza kuona sehemu zote na kuwa madereva wenye magari wanaweza kukuona. Endelea kuvuka kwa kutumia Kanuni za Uvukaji. Usisimame mbele au nyuma ya gari lolote lililosimama ambalo injini yake haijazimwa.

Wakati wa usiku, vuka karibu na taa za mtaani. Iwapo hakuna taa za barabarani, alama za pundamilia au kizingwa ambavyo unaweza kuvitumia, vuka karibu na taa za mtaani, ili madereva waweze kukuona kwa urahisi zaidi. Vaa nguo zenye rangi inayoangaza au kung'aa ili kufanya wengine wakuone kwa urahisi wakati wa usiku.

Kamwe usivuke barabara moja kwa moja nyuma au mbele ya basi. Usivuke barabara na basi – acha mpaka lipite, ili uweze kuona pande zote mbili za barabara vizuri.

Usivuke mbele ya magari ya dharura. Iwapo utayaona au kuyasikia magari ya wagonjwa, magari ya kuzima moto, ya polisi au magari

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:8 9/25/08 3:14:40 PM

mengine yoyote ya dharura yenye vimulimuli na sauti za ving'ora, usivuke barabara mpaka yapite.

Kuvuka na watoto. Watoto wadogo hawajui jinsi barabara ilivyo hatari, na si wajuzi wa kuamua juu ya kasi na umbali. Kwa sababu ni watoto ni rahisi kuchanganywa, na wanaweza kufanya vitu vya hatari. Usiwaache watoto wadogo kuvuka barabara peke yao. Mara zote shika mikono yao kwa nguvu wakati wa kuvuka. Watoto hujifunza kwa mifano, kwa hiyo wakati wote tumia Kanuni za Uvukaji wakati wa kuvuka barabara, na waelezee.

Sheria za waendesha baiskeli

Mwongozo wa jumla

Fuata sheria za barabarani. Kwa kawaida fuata sheria zilezile za barabarani zinazotumiwa na madereva wa magari. LAZIMA ufuate alama zote za barabarani, ishara, michoro na maelekezo yanayotolewa na maofisa wa polisi. USIENDESHE kwenye mazingira ya hatari, bila kuwa makini au bila kujali.

Chagua ukubwa sahihi wa baiskeli. Kwa uzuri na usalama hakikisha kuwa baiskeli si kubwa sana au ndogo sana kwako.

Chagua baiskeli yenye hali nzuri za taa na viashiria. Madereva wanapata shida kuwaona waendesha baiskeli, hasa usiku. Viashiria vizuri mfano vile vinavyowekwa kwenye pedeli, vitakusaidia kuonekana kwa urahisi zaidi.

Mara zote iweke baiskeli yako katika hali nzuri. Hakikisha kuwa:
- Taa na viashiria ni safi na vinafanya kazi vizuri
- Matairi yako katika hali nzuri na yamejazwa upepo kulingana na ushauri wa kiwanda kilichoitengeneza
- Breki na gea vinafanya kazi vizuri
- Mnyororo umekaa vizuri na kuwekwa mafuta
- Kiti kimerekebishwa kwenye urefu sahihi.

Tumia kengele. LAZIMA ufunge kengele kwenye baiskeli yako na uitumie wakati unaofaa kuwaonya watumiaji wengine wa barabara kuwepo kwako.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:9 9/25/08 3:14:41 PM

Kuendesha baiskeli usiku. Wakati wa usiku LAZIMA utumie taa (nyeupe mbele, nyekundu nyuma). Baiskeli yako LAZIMA iwe na kiashiria chekundu nyuma.



Vifaa vya Usalama na Mavazi. Tumia/vaa mavazi ya kujikingia kama vile helmeti ya baiskeli iliyowekwa vizuri ambayo itakuwezesha kugundua viwango vya usalama. Epuka kuvaa makoti marefu ambayo yanaweza kuingia kwenye mnyororo au matairi. Mara zote vaa nguo zinazong'aa au za rangi, hasa jaketi linaloweza kuonekana sana la njano na mistari inayoakisi. Nguo zenye alama mikononi au kwenye vifundo pia husaidia.



Angalia – ashiria - tenda. Angalia nyuma yako kabla ya kuondoka, kulipita gari, nenda katikati ya barabara pinda kulia, na kusimama. Angalia kuwa hakuna kitu kinachokuja. Kisha toa ishara nzuri ya mkono kuonyesha kusudio lako, na uendeshe kuelekea huko.

Uendeshaji salama. Wakati unaendesha:



- Weka mikono yote miwili kwenye usukani isipokua wakati wa kutoa ishara
- Weka miguu yote miwili kwenye pedeli
- Usijishikilie kwenye magari au baiskeli nyingine
- Usiendeshe ukiwa karibu nyuma ya gari
- Usibebe abiria isipokuwa kama baiskeli yako imetengenezwa kubeba abiria mmoja
- Usibebe kitu chochote ambacho kitakupa ugumu wa kuendesha baiskeli
- Endesha upande wa kushoto wa barabara karibu na ukingo
- Endesha kwenye mstari mmoja (mmoja nyuma ya mwingine).

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:10 9/25/08 3:14:41 PM

Huko vijijini unaweza kuendesha kwenye njia za vijijini, lakini kwa mwendo mdogo. Chukua tahadhari kubwa usiwape taabu au kuwaathiri watembeao kwa miguu.



Vizuizi. Angalia mbele vizuri ili kuona vizuizi mfano mashimo, mabwawa ya maji na magari yaliyoegeshwa, ili usilazimike kupinda haraka kuvikwepa. Acha nafasi ya kutosha wakati unayapita magari yaliyoegeshwa, na uwe makini na milango iliyofunguliwa kwenye njia yako. Uwe makini unapokuwa karibu na matuta ya barabarani, barabara nyembamba na mazingira mengine yasiyo mazuri ya barabara - usiendeshe kwenye mtaro wa maji au kwenye njia ya waenda kwa miguu ili kuwazunguka.

Usinywe na kuendesha. USIENDESHE ukiwa umelewa dawa za kulevya, pombe au aina yoyote ya vileo.

Tumia njia ya baiskeli kama ipo. Njia ya baiskeli inaweza kuonyeshwa kwa mistari ya njano na alama ya baiskeli. Endesha kwenye njia hiyo na angalia magari yanayoacha barabara au kuingia barabara za pembeni. Katika barabara nyingine kuna njia za baiskeli ambazo zinatenganishwa na barabara kuu. Pale njia hizo zinapokuwa zinachangiwa na watembea kwa miguu endesha kwenye upande ulioonyeshwa kwa ajili ya waendesha baiskeli na chukua tahadhari usiwape shida au kuwasumbua watembeao kwa miguu.

Njia za mabasi. Mwendesha baiskeli anaweza tu kutumia njia ya basi iwapo alama ya barabarani inajumuisha alama ya baiskeli. Uwe makini sana wakati wa kulipita basi au wakati wa kutoka kwenye njia ya basi.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:11 9/25/08 3:14:42 PM

Usiiache baiskeli yako mahali ambapo inaweza kuwa kizuizi. Acha baiskeli yako katika mahali pa salama. Tumia vyombo vya kuegeshea baiskeli iwapo vinapatikana.

Makutano ya barabara

Punguza mwendo na kuwa makini zaidi kwenye makutano kwa sababu madereva wanaweza wasikuone. Kamwe usiamini kuwa madereva wanakuona. Iwapo utaona kuwa makutano hayo yana magari mengi na vigumu kupita, simama na ushuke – kisha tembea na baiskeli yako kuvuka barabara, fuata sehemu ambayo watembea kwa miguu wengine wanapita.

Angalia magari yanayopinda mbele yako. Angalia madereva wanaotoka pembeni mwa barabara – wanaweza wasikuone. Usiendeshe upande wa magari yanayoashiria au kupunguza mwendo kupinda kushoto – madereva wa magari makubwa na marefu wakati mwingine hushindwa kuona kuwa wamekupita vizuri kabla ya kupinda kushoto.

Kupinda kulia. Unapopinda kulia, angalia magari yaliyo nyuma yako, onyesha ishara inayofaa, na iwapo ni salama nenda katikati ya barabara. Subiri hadi kunapokuwa na upenyo ambao ni salama barabarani kabla ya kumalizia kupinda.

Mzunguko. Chukua tahadhari kubwa kwenye mzunguko kwani mara nyingi madereva hushindwa kuwaona na kuwaruhusu waendesha baiskeli. Kwa ujumla ni salama kukaribia mzunguko kwa njia iliyo upande wa kushoto na kuendelea kupita kushoto kwenye mzunguko hicho – chukua tahadhari kubwa wakati unaendesha kupitia sehemu ya kutokea, na unaweza kuhitaji kuashiria kulia kuwaonyesha madereva kuwa hutoki kwenye mzunguko. Angalia magari yanayokatisha kwenye njia yako kuondoka au kuingia kwenye mzunguko. Mara zote ni salama kuyaacha magari marefu kupita kwenye mzunguko kabla ya kuendelea.

Iwapo huna uhakika unaweza kuendesha kwa usalama kwenye mzunguko, simama na shuka kwenye baiskeli na utembee nayo kwenye njia ya watembea kwa miguu. Tumia Kanuni za Uvukaji wakati unapita kwenye barabara ya kuingilia.

Ishara zinazoongoza makutano. Fuata maelekezo yanayotolewa na ishara ya taa za barabarani. LAZIMA usimame iwapo ishara ya

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:12 9/25/08 3:14:42 PM

taa nyekundu au za njano itaonyeshwa. Simama kwenye sehemu iliyoandikwa SIMAMA au fuata nafasi yako kwenye mstari wa magari yanayosubiri.

Kuvuka barabara

Usiendeshe baiskeli kupita kwenye alama za pundamilia au ishara inayowaongoza watembea kwa miguu - shuka na vuka ukitembea na baiskeli yako.

Chukua tahadhari kubwa wakati unavuka au kupinda kwenye barabara mbili kwa vile vyombo vya usafiri kwa kawaida vitakuwa vinakwenda kasi sana. Subiri kupata upenyo ulio salama na vuka kila barabara.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:13 9/25/08 3:14:42 PM

Sheria za abiria anayetumia mabasi, daladala, teksi na pikipiki

Usalama wako kwa kiasi kikubwa uko mikononi mwa dereva, lakini kuna mambo unayoweza kufanya yatakayosaidia safari yako kuwa ya usalama:

Daima:

- Subiri mabasi, daladala na teksi vikupakie mahali pa salama, mfano kwenye vituo maalum vya mabasi na teksi
- Subiri gari pembeni mwa barabara - si barabarani
- Subiri gari isimame kabisa kabla ya kupanda au kushuka
- Daima subiri abiria wengine washuke kwanza kabla hujapanda
- Uwe makini wakati unafungua mlango wa gari – unaweza kumgonga mtu
- Shuka kwenye gari tu kwenye vituo vinavyotambulika pembeni mwa barabara
- Tumia mkanda wa usalama kwenye kiti kama upo.

Kamwe usifanye mambo yafuatayo:

- Kupanda kwenye gari linaloonekana kuwa bovu na limechakaa
- Kupanda pikipiki ambayo tayari imebeba abiria
- Kuwasukuma wengine wakati wa kupanda au kushuka kwenye gari
- Kumsumbua dereva au kumzonga
- Kumshawishi dereva kuendesha kwa kasi au kwa hatari
- Kuingilia vifaa vya gari (ikiwa ni pamoja na mifumo ya viyoyozi na muziki)
- Kukaa wakati kichwa au mkono wako ukiwa nje ya dirisha – unaweza kujeruhiwa vibaya na gari linalopita.
- Kuning'inia nje ya gari
- Kusafiri ukiwa nje ya gari – ni hatari sana kuliko kuwa ndani
- Kukaa mbele iwapo wewe ni mtoto mdogo
- Kukaa mbele iwapo umebeba mtoto mchanga au mtoto mdogo
- Kutupa vitu nje kupitia dirishani
- Kupokea chakula au kinywaji kutoka kwa wageni/watu usio wafahamu
- Kuvuka barabara ghalfa mbele au nyuma ya gari - madereva wa magari mengine hawataweza kukuona
- Kusafiri nyuma ya magari madogo ya mizigo, malori na magari mengine yaliyotengenezwa kubeba mizigo tu – ni hatari sana.
- Kupanda magari ambayo tayari yamejaa.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:14 9/25/08 3:14:42 PM

Washawishi madereva kuendesha kwa usalama na umakini. Walalamikie katika namna nzuri, kama wanaendesha kwa hatari, ukiwaona wanakunywa vileo, au wanamruhusu dereva msaidizi asiye na ujuzi. Kama hawajiheshimu, shuka kwenye kituo kinachofuata, andika namba ya usajili ya gari na waarifu polisi. Bora upoteze fedha/nauli ulizolipa kwa safari kuliko kupoteza uhai wako.


Mkataze dereva au msaidizi wake iwapo wanajaribu kupakia abiria wakati gari tayari limejaa.

Sheria za watu wanaochunga wanyama

LAZIMA umdhibiti vizuri mnyama yeyote unayemchunga. Hili lifanyike kama una mnyama mmoja au kundi.

Iwapo kuna wanyama wengi muwe watu wawili, mmoja mbele na mwingine nyuma. Katika sehemu za hatari mfano kwenye kona kali na kwenye vilima vikali mmoja aende mbele kabisa kuwaonya watumiaji wengine wa barabara. Kwenye barabara za magari yaendayo kasi muwe pia na mtu mwenye bendera kuyaonya magari yanayokaribia – mmoja awe m100 mbele ya wanyama, na mwingine awe m100 nyuma ya wanyama. Kamwe usichunge wanyama barabarani usiku.

LAZIMA uwe na kibali cha Polisi kama unataka kuchunga wanyama zaidi ya 50 kwenye barabara yoyote au mtaa.



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:15 9/25/08 3:14:43 PM

Sheria za madereva wa magari

Kabla ya kuendesha

- LAZIMA uwe na leseni halali ya udereva kwa daraja la gari unaloendesha (unaweza kuendesha kwa kutumia leseni halali ya kimataifa au leseni ya kigeni kwa miezi sita baada ya kufika Tanzania kwa mara ya kwanza).
- LAZIMA uwe unajisikia vizuri - usiwe mgonjwa au umechoka.
- LAZIMA uweze kuona vizuri (uweze kusoma kibao cha namba za gari kutoka umbali wa mita 20) - iwapo unahitaji kuvaa miwani au lenzi ili kuona LAZIMA uvae wakati wa kuendesha - usitumie miwani ya jua usiku au kukiwa na mwanga mdogo.
- USISHINDWE kuliongoza gari kwa sababu ya kunywa pombe au kutumia dawa za kulevya njia pekee ya kuwa na uhakika na jambo hili ni kutokunywa pombe au kutumia dawa yoyote ya kulevya.
- LAZIMA uhakikishe kuwa, wakati watoto wadogo wamo kwenye gari, wawe viti vya nyuma ya gari, wako chini ya usimamizi wa watu wazima, na milango imefungwa (tumia vidhibiti mtoto) – inashauriwa kuwa uweke na kutumia vizuizi vya mtoto vinavyofaa (kibebea mtoto, kiti cha mtoto, au kiti cha busta kwa watoto wakubwa).
- LAZIMA ujifunge mkanda – hili lifanywe na abiria wa kiti cha mbele pia – inashauriwa sana kuwa abiria wa viti vya nyuma pia wajifunge mikanda.
- LAZIMA urekebishe kiti chako na vioo ili uweze kuendesha vizuri, na uweze kuona sehemu zote za gari.

LAZIMA uchukue:
- leseni yako ya udereva
- cheti halisi cha usajili wa gari au nakala halisi

LAZIMA ubandike kwenye gari:
- kibandiko/stika ya leseni halali ya gari
- kibandiko/stika ya bima

(isipokuwa kwa magari yanayomilikiwa na Serikali)

Gari lako LAZIMA:
- liwe katika hali nzuri ya kiufundi
- liwe ndani ya eneo linaloruhusiwa
- liendane na viwango vyote, vya utengenezaji (Shirika la Viwango Tanzania)
- liendane na kikomo cha idadi ya abiria ambao wanaweza kubebwa

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:16 9/25/08 3:14:43 PM

- lipakie mizigo kiusalama, kulingana na kanuni – hakikisha kuwa mizigo yoyote iliyobebwa iko salama na isining'inie nje na isisababishe hatari – weka alama ya tahadhari mwishoni mwa mzigo uliozidi sehemu ya nyuma ya gari.
- Lilingane na kanuni za kiwango cha juu cha uzito.

Ukaguaji wa kila siku (magari)

- Kagua magurudumu kama yako kwenye hali nzuri na nati ziko salama
- Kagua kuona kuna mafuta ya kutosha, mafuta ya breki, maji, na kiosha kioo cha mbele
- Kagua kuwa waipa za kioo cha mbele zinafanya kazi
- Kagua matairi, ikiwa ni pamoja na tairi la akiba, kwa uharibifu, kina cha tredi (kima cha chini kilichopendekezwa ni: mm3) na upepo
- Kagua kuwa taa na indiketa zinafanya kazi vizuri
- Kagua kuwa honi inafanya kazi vizuri
- Kagua kuwa vioo vyote ni safi ndani na nje, na kuwa vioo na viashiria ni safi
- Kagua nje ya gari kwa ubovu au uharibifu
- Kagua kuwa vifaa na jeki vipo na vinafanyakazi vizuri
- Kagua kama kuna mngurumo usio wa kawaida wakati injini inafanya kazi.

Usiendeshe wakati umechoka au unaumwa. Kuendesha kunaweza kukufanya ujisikie usingizi. Hili linaweza kuepukwa kwa kuhakikisha kuwa kuna hewa ya kutosha kwenye gari lako. Iwapo unajisikia kuchoka wakati wa kuendesha tafuta sehemu salama ya kusimama na pumzika. Kunywa vikombe viwili vya kahawa kunaweza kukusaidia. Inashauriwa kuwa upumzike kwa dakika 30 kila baada ya kuendesha kwa saa 3. Usiendeshe kwa zaidi ya saa 9 kwa siku. Epuka kuanza safari ndefu usiku sana. Madereva wa magari ya biashara lazima wafuate kanuni za saa za madereva.

Usiendeshe wakati unaumwa. Iwapo unameza dawa muulize daktari wako au mfamasia kama ni salama kuendesha. Iwapo utakuwa mgonjwa kwa muda mrefu au hujiwezi na daktari wako akisema si salama tena kwako kuendesha ipeleke leseni yako Polisi.


Usinywe pombe na kuendesha. Pombe hupunguza mpangilio wako, kupunguza utendaji wako, kuathiri uamuzi wako wa mwendo, umbali na hatari, na kukupa hisia zisizo sahihi za kujiamini. Hairuhusiwi kuendesha

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:17 9/25/08 3:14:43 PM

ukiwa na kiasi cha pombe kwenye damu cha juu zaidi ya mg80/ml100, lakini uendeshaji wako unaweza kuathiriwa kabla hata ya kufikia kikomo hiki. Kwa hiyo, ni vizuri kutokunywa kileo chochote kabla ya kuendesha. Kumbuka kuwa inachukua muda kwa kileo kuondoka mwilini mwako, hivyo unaweza kutokuwa katika hali nzuri ya kuendesha jioni baada ya kunywa pombe wakati wa chakula cha mchana. Madereva wa mabasi, daladala, na magari ya mizigo yanayotoa huduma za usafiri WASINYWE kileo chochote kabla ya kuendesha.

Iwapo unajifunza udereva. LAZIMA uwe na leseni halali ya dereva mwanafunzi, na wakati unaendesha LAZIMA uwe unaongozwa na mwalimu wa udereva aliyesajiliwa anayefanya kazi kwenye shule ya udereva iliyothibitishwa. Iwapo unajifunza kuendesha pikipiki, skuta au baiskeli mota lazima uchukue mafunzo ya msingi kwenye shule ya udereva iliyothibitishwa kabla ya kuendesha barabarani - usibebe abiria nyuma. Magari yote (pamoja na pikipiki na baiskeli mota) yanayoendeshwa na mwanafunzi LAZIMA yawe na kibao cha Mwanafunzi (L) kilichothibitishwa.

Ushauri kwa waendesha pikipiki. Dereva wa pikipiki au skuta LAZIMA avae helmeti ya usalama iliyothibitishwa ambayo imefungwa kiusalama. Inashauriwa sana kuwa abiria wa nyuma pia avae helmeti. USIBEBE zaidi ya abiria mmoja.



Waendeshaji wote wanashauriwa kuvaa vikinga macho, na mabuti magumu, glovu, na nguo ambazo zitakukinga iwapo utaanguka. Abiria wa kiti cha nyuma lazima wakae kwa kutanua miguu kwenye kiti halisi na kuweka miguu yote miwili kwenye sehemu ya kukanyagia. Daima vaa nguo zinazong'aa au zenye rangi au rangi angazi, zinazopendelewa zaidi jaketi la njano linaloonekana vizuri lenye mistari inayoakisi. Inashauriwa kuwa upunguze nuru ya taa mchana, kwani hili litafanya uonekane zaidi.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:18 9/25/08 3:14:44 PM

Wakati wa kuendesha


Endesha kwa usalama. USIENDESHE kwa hatari au kwa uzembe. Hii huelezwa kama tabia ambayo dereva mwenye ujuzi ataichukulia kama hatari – mfano kulipita gari jingine mahali ambapo pana kona kali kiasi kuwa huwezi kuona vizuri mbele.

Endesha kwa umakini. USIENDESHE bila kujali. Lazima uwe macho na uchukue tahadhari wakati wote. Ni kutokuwa makini kuruhusu kusumbuliwa wakati unaendesha, au kutoangalia vizuri kama barabara haina kikwazo kabla ya kuingia.

Wathamini wengine. Usiendeshe kama vile uko kwenye mashindano na madereva wengine. Endesha kwa utulivu na kuwa mvumilivu iwapo wengine watafanya makosa. Usilazimishe magari madogo yakupishe.

Kuwa mwangalifu – usisumbuliwe. Epuka kuzungumza au kubishana na abiria. Usile, usinywe, usisome au kuvuta sigara wakati unaendesha – Usitumie simu ya mkononi wakati unaendesha hata kama una kifaa cha kuifanya mikono isitumike. Tafuta sehemu nzuri usimame, na kisha tumia simu yako.

Endesha kwa kuangazaangaza wakati wote. Usiangalie sehemu moja kwa zaidi ya sekunde 2 – endelea kuangaza sehemu zote kuhakikisha kuwa hukosi kuona kitu chochote – angalia – na kila sekunde 5 angalia kwenye vioo vyako, hata kama unadhani hakuna magari karibu.




Endesha kwa Kujihami. Angalia nje kutafuta uwezekano wa kutokea matatizo mbele, mfano mtoto anayechezea mpira, au gari linakuja kwa kasi pembeni mwa barabara. Iwapo kuna gari pembeni mwa barabara

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:19 9/25/08 3:14:44 PM

lenye dereva ndani, tegemea litaingia mbele yako ghafla. Iwapo basi limesimama mbele yako, jitayarishe kwa abiria kuvuka barabara kutoka nyuma yake. Iwapo utaona uwezekano wa tatizo kama hili punguza mwendo na jiandae kuchukua hatua kuepuka kugongana.

Tumia ishara kuwaonya na kuwaarifu watumiaji wengine wa barabara. LAZIMA utumie viashiria vya mwelekeo au ishara ya mkono kabla ya kubadili mwendo au mwelekeo, kusimama au kuondoka. Toa ishara inayoeleweka kwa muda wa kutosha, na kumbuka kuacha baada ya kitendo husika.



Tumia honi tu iwapo ni lazima uwaonye watumiaji wengine wa barabara kuwa uko pale. Iwapo madereva watatumia honi kupita kiasi, watumiaji wa barabara hawatazisikiliza. Usitumie honi "Kusalimia" au kuonyesha umekasirishwa na mtu, au kumueleza dereva aliye mbele kuharakisha na kuongeza mwendo. Usitumie honi nje ya hospitali, mahakamani na shuleni, au kati ya saa 5 usiku na saa 12 asubuhi mjini. Epuka kutumia honi kwenye Hifadhi za Taifa na Mbuga za Wanyama.

Washa taa zako ghafla pale utakapotaka kuwajulisha watumiaji wengine wa barabara wajue kuwa upo, katika mazingira ambayo honi inaweza kutosikika au mjini wakati wa usiku. Usiwashe taa zako ghafla kuonyesha kuwa umekasirika au kujaribu au kudai haki ya njia. Iwapo dereva mwingine atakuwashia taa ghafla, usiichukulie kuwa ni ishara ya kukuruhusu kupita.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:20 9/25/08 3:14:44 PM

Fuata alama za barabarani. LAZIMA ufuate alama zote za barabarani, na ishara na michoro ya barabarani. Hakikisha kuwa unajua na kutenda kulingana na alama na michoro yote mingine ya barabarani. Sehemu ya mwisho ya Kanuni hizi za Barabara inaonyesha alama zote. LAZIMA pia ufuate ishara zinazotolewa na maofisa wenye sare wa polisi na watu wengine wenye mamlaka. Ishara zao zinazidi alama na michoro yote mingine.

Alama za maofisi wa Polisi au watu wengine wenye mamlaka



SIMAMA Askari wa barabarani anayeashiria kwa mbele



SIMAMA Askari wa barabarani anayeashiria kwa nyuma



SIMAMA Askari wa barabarani anayeashiria mbele na nyuma



SIMAMA Askari wa barabarani anayeashiria kwa upande mmoja



PITA



PITA


Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:21 9/25/08 3:14:45 PM

Kuondoka / kuendesha. Kabla ya kuondoka, daima tumia vioo vyako, ishara na tazama nyuma ya mabega yako kuona kuwa barabara haina kikwazo. Ondoka iwapo umejiridhisha kuwa ni salama kufanya hivyo.

Pita kushoto. LAZIMA uendeshe upande wa kushoto wa barabara. Vyombo vinavyokwenda polepole (baiskeli, mikokoteni inayokokotwa na ng'ombe, kwa mikono na matrekta, n.k) lazima vipite upande wa kushoto na kuruhusu magari yaendayo kasi kuvipita.

USIENDESHE kwenye njia ya watembea kwa miguu au maeneo ya watembea kwa miguu.

Vioo – alama – kitendo. Tumia vioo vyako daima ili wakati wote ujue kilichoko nyuma na pembeni yako. Tumia vioo vyako vizuri kabla ya kupinda au kubadili nafasi/njia, na kisha toa ishara ifaayo.



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:22 9/25/08 3:14:45 PM

Waendesha pikipiki wanashauriwa kuangalia nyuma yao kabla ya kubadili njia na kupinda kulia.

Usiweke msururu wa magari nyuma yako. USIENDESHE taratibu bila sababu. Iwapo unaendesha gari kubwa au linalokwenda polepole na kuna foleni ya magari nyuma yako, LAZIMA utafute sehemu uingie kwa usalama na kuruhusu magari mengine yakupite.

Endesha kwenye njia. Pale penye njia zaidi ya moja zenye mwelekeo mmoja, tumia njia ya kushoto kwenda mbele na nyingine kwa ajili ya kuvipita vyombo vingine, kupinda kulia, au kuyapita magari yaliyosimama. Usibaki kwenye njia ya kulia muda mrefu zaidi ya unaohitajika. Wakati wa kubadili njia kumbuka vioo – ishara – kitendo

Foleni ya magari. Iwapo kuna mstari wa magari yaliyosimama mbele, jiunge nyuma yake. Usiivuke foleni. Kuwa mvumilivu. Daima simamisha gari lako ili uweze kuyaona matairi ya nyuma ya gari la mbele – linaweza kurudi nyuma kidogo wakati linaanza kuondoka. Iwapo utafika kwenye alama za pundamilia ukiwa kwenye foleni usisimame kwenye alama hizo – acha ili waendao kwa miguu waitumie.

Mwendo


Endesha kwa mwendo salama. USIENDESHE kwa mwendo ambao unaweza kuwa wa hatari kwa wengine. Daima rekebisha mwendo wako kulingana na mazingira. Kwa mfano, punguza mwendo kama unakaribia kona, daraja jembamba, au makutano, au eneo lenye waenda kwa miguu wengi. Chagua gea itakayokuwezesha kulidhibiti gari zaidi. Endesha polepole zaidi iwapo barabara ina majimaji, au huwezi kuona vizuri.

Endesha polepole zaidi usiku, kama ni vigumu kuwaona watembea kwa miguu, waendesha baiskeli, wanyama, na magari yaliyoegeshwa au kuharibika.

Kuendesha kwenye barabara zisizo na lami. Daima endesha polepole zaidi kwenye barabara zisizo na lami, nyonga usukani polepole, na epuka kufunga breki kwa nguvu. Barabara zisizo na lami zinateleza zaidi ya zenye lami, na matairi yako yanaupungufu wa asilimia 50 ya kiwango cha ukandamizaji.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:23 9/25/08 3:14:46 PM

Endesha katika namna ya kusimama wakati wote kuepuka kugonga kitu chochote. Endesha katika mwendo utakaokuruhusu kusimama vizuri katika umbali unaouona kufaa. Usiendeshe kwa kasi kwenye kona au juu ya kilele cha mlima – itakuwaje iwapo gari litaharibika mahali ambapo huoni vizuri? Kumbuka kuwa, ukiongeza mara dufu mwendo wako, umbali wako wa kusimama unaongezeka mara tatu – angalia mchoro. Umbali wa kusimama utakuwa mrefu zaidi ya huu kwenye barabara zenye majimaji zisizo na lami. Magari makubwa na pikipiki daima huchukua muda mrefu kusimama kuliko magari madogo.



Kama kanuni ya jumla daima acha nafasi ya sekunde – 2 kati ya gari lako na lililo mbele yako. Moja ya njia inayotumika kupima nafasi hii wakati wa kuendesha ni kuhesabu “elfu moja na moja, elfu moja na mbili” wakati gari lililo mbele yako litakapopita sehemu iliyowekwa - Iwapo utapita mahali palipowekwa kabla ya kumaliza hesabu yako, uko karibu mno.

Fuata ukomo wa mwendo. USIPITISHE mwendo wa kiwango cha juu wa gari lako. Kwa sasa ukomo wa mwendo kisheria ni:

Km 50 kwa saa kwa magari yote kwenye maeneo ya makazi (hata kama hakuna alama ya barabarani)

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:24 9/25/08 3:14:46 PM

Km 80 kwa saa kwa magari makubwa ya mizigo (> uzito halisi wa gari wa kg 3500) na magari ya huduma za umma (mabasi, mabasi ya safari ndefu, lakini si teksi) nje ya maeneo ya makazi
Km 100 kwa saa ni mwendo unaoshauriwa,wa juu kwa magari madogo na magari mengine ya wastani katika eneo la makazi.

Mwendo huu unaweza kutofautiana kulingana na alama ukomo za barabarani za maeneo husika. USIZIDISHE mwendo wa mwisho wa juu zaidi ya unaoonyeshwa kwenye alama. **Kumbuka kuwa ukomo wa mwendo haumaanishi kuwa daima itakuwa salama kuendesha katika mwendo huo.** Lazima uendeshe katika mwendo ambao ni salama kwa barabara hiyo, watumiaji wengine wa barabara na hali ya hewa.

Kulipita gari jingine

Kabla ya kulipita gari jingine LAZIMA uhakikishe kuwa:
- barabara haina vikwazo vyovyote
- gari lililo nyuma halijaanza kulipita gari lako
- gari la mbele halijaanza kulipita gari jingine
- kuna upenyo mkubwa wa kutosha mbele ya gari unalotaka kulipita.

Usilipite gari jingine isipokuwa kama una uhakika unaweza kufanya hivyo bila ya kusababisha hatari kwa watumiaji wengine wa barabara au kwako mwenyewe. Iwapo una shaka usilipite gari jingine.


Usilipite gari linalotembea au lililoegeshwa:
- iwapo gari linakaribia kutoka upande mwingine – isipokuwa kama una uhakika unaweza kufanya hivyo bila ya kulilazimisha gari hilo kupunguza mwendo au kupinda ghafla ili kukuepuka
- pale gari linalopitwa linaashiria kupinda kulia
- pale ambapo huwezi kuona umbali wa kutosha mbele, mfano kwenye kona au karibu ya kilele cha kilima
- kwenye makutano
- kwenye alama za pundamilia au karibu na alama hizo au mahali pengine wanapovuka watembea kwa miguu
- kwenye reli au karibu na reli
- ambapo unatakiwa kuingia kwenye njia iliyo maalum kwa mabasi au waendesha baiskeli
- ambapo unatakiwa kupita kwenye eneo lenye mistari ya mshazari au ya umbo la V.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:25 9/25/08 3:14:46 PM

- ambapo kulipita gari jingine hakuruhusiwi kwa alama ya “Hakuna kulipita gari jingine” au michoro ya barabarani.


Michoro ya barabarani ambayo inakuonyesha mahali ambapo unaweza kulipita gari jingine.

Iwapo mstari mweupe wa katikati ya barabara umechorwa kwa kukatikakatika (- - - -) unaweza kuvuka ili kulipita gari jingine, kama ni salama kufanya hivyo. Iwapo mstari mweupe wa katikati ya barabara haujakatikakatika (_____), USIVUKE mstari huo, isipokuwa kama ni muhimu kulipita gari lililosimama au kupinda kwenye barabara ya upande mwingine. Pale ambapo pana mistari miwili ya kati mstari ulio karibu na wewe ndio utakaoutumia.




Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:26 9/25/08 3:14:46 PM

Sehemu zisizo salama kulipita gari jingine



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:27 9/25/08 3:14:47 PM

Utaratibu wa msingi wa kulipita gari jingine.
Kabla hujaanza kulipita gari hakikisha kuwa barabara haina vikwazo mbele kukuwezes ha kulipita gari na kurudi kushoto bila ya kulilazimisha gari jingine kupunguza mwendo au kupinda haraka ili kukukwepa. Kama una shaka – usilipite gari jingine. Tumia vioo vyako kuona kuwa hakuna gari linalokupita. Toa ishara kabla ya kuanza kutoka **[1]**. Kuwa mwangalifu zaidi usiku na kwenye ukungu au mvua kubwa wakati inapokuwa vigumu kuamua kuhusu mwendo na umbali.
Kumbuka: vioo-ishara-tendo.



Iwapo huna hakika na kile ambacho dereva wa gari la mbele atafanya, piga honi.

Unapokuwa umeanza kulipita gari jingine, **[2]** nenda haraka kulipita gari hilo na liache kwa umbali fulani. Unapozipita baiskeli au pikipiki vipatie angalau umbali zaidi kuliko ule wa gari. Rudi upande wa kushoto wa barabara haraka iwezekanavyo, **[3]** lakini usirudi haraka kiasi kuwa gari unalolipita kulazimika kufunga breki au kupinda haraka ili kukukwepa. Fanya hivi kwa kuliangalia gari kwenye kioo chako.

Iwapo gari lingine litakuwa linakupita. Usiongeze mwendo wako unapokuwa unapitwa. Elekea kushoto kama unaweza kufanya hivyo kwa usalama. Punguza mwendo ikibidi kuliacha gari linalokupita lipite haraka na kwa usalama.

Lipite gari lingine upande wa kulia. Daima lipite gari jingine upande wa kulia, isipokuwa kama:

- gari la mbele yako linaonyesha ishara ya kupinda kulia, na kuna nafasi ya kulipita kwa usalama kushoto (usiendeshe kwenye njia ya waendao kwa miguu);

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:28 9/25/08 3:14:48 PM

- magari yanakwenda polepole kwenye njia na magari kwenye njia ya kulia yanakwenda polepole zaidi yako.


Pale wengine watakapokuashiria upite. Wakati mwingine dereva wa gari la mbele yako anaweza kukuashiria kuwa barabara haina vikwazo kwako kupita. Usidhani kuwa dereva yuko sahihi. Lipite gari hilo tu pale utakapoona kuwa barabara haina kikwazo chochote.

Iwapo gari unalolipita litaongeza mwendo au kuonyesha kukataa kwa namna yoyote, acha kujaribu kulipita. Usishindane kamwe na dereva mwingine.

Makutano

Kukaribia makutano ya barabara. Kugongana kwingi hutokea kwenye makutano, hivyo chukua tahadhari zaidi. Angalia makutano yaliyo mbele yako, na fikiria hatua ipi ya kuchukua, iwapo utatakiwa kufanya hivyo. Hakikisha kuwa gari lako liko mahali sahihi kwa hatua unayotaka kuichukua na kuwa unaendesha kwa mwendo unaofaa.

Kaa kwenye njia au mahali sahihi. Iwapo barabara itakuwa na alama za njia, ingia kwenye njia sahihi kwa wakati mzuri. Fuata mishale inayoonyesha njia ipi ni ya mwelekeo upi. Usibadili njia bila sababu ya msingi. Iwapo kuna foleni ya magari mbele yako, usijaribu kuivuka foleni hiyo – kuwa mvumilivu.



Fuata kanuni za kipaumbele.
Kwenye makutano yenye alama ya “SIMAMA” (pia itakuwa na mstari mweupe usiokatikakatika wa “SIMAMA” kukata barabara) LAZIMA usimame kabisa kwenye mstari huo. Angalia kwa makini kuona kama kuna gari lolote linalokuja. Subiri upate upenyo salama kabla ya kupita.

Kwenye makutano yenye alama au mchoro wa “KURUHUSU” (mstari mweupe uliokatikakatika kukata barabara) LAZIMA uyaruhusu magari ya kwenye barabara nyingine. Subiri upate upenyo salama, kabla ya kupita – usiyalazimishe magari mengine kupunguza mwendo haraka au kukukwepa ghafla.


Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:29 9/25/08 3:14:49 PM


Pale ambapo hakuna alama na mchoro wowote, daima kumbuka kuyaruhusu magari yanayotoka kulia.

Pale ambapo una haki ya kupita, nenda mbele kwa tahadhari na uwe tayari, ikibidi, kupunguza mwendo na kusimama kuepuka kugongana.

Usiingie kwenye makutano hadi njia yako itakapokuwa haina vikwazo. Usisite kwenye makutano bila ya ulazima. Subiri na ruhusu magari mengine yapite mbele yako. Kama madereva watakuwa wavumilivu na kutumia maarifa yao ya kawaida, kila mmoja atafika anakokwenda kwa haraka zaidi.

Haki za msingi za njia






Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:30 9/25/08 3:14:49 PM

Kupinda kulia

1. Hakikisha usalama kabla ya kupinda kulia, tumia vioo vyako kuona kuwa magari yaliyo nyuma yako umbali salama
2. Onyesha ishara ya kupinda kulia na anza kwenda polepole
3. Nenda kwenye sehemu ya kushoto ya katikati ya barabara
4. Mara tu panapokuwa na upenyo salama wa magari yanayokuja pinda kulia-usipite njia ya mkato kwenye kona.



Angalia waendesha baiskeli, pikipiki, watembea kwa miguu – iwapo kuna watembea kwa miguu wanaovuka barabara kwenye sehemu unayoelekea kupinda, lazima usimame na kuwaacha wapite.


Waangalie watumiaji wengine wa barabara, hususan waendesha pikipiki, baiskeli na watembea kwa miguu, na wajulishe kile unachotaka kufanya kwa kuonyesha ishara ya wazi.

Yaruhusu magari marefu kupinda. Yanaweza kutumia upana wote wa barabara ili kupinda.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:31 9/25/08 3:14:50 PM

Kupinda kushoto

1. Hakikisha usalama kabla ya kupinda kushoto, tumia vioo vyako kuona kuwa hakuna gari linalokuja kushoto kwako nyuma.
2. Onyesha ishara ya kupinda kushoto na anza kwenda polepole.
3. Kama barabara haina vikwazo pinda huku ukiwa karibu na ukingo wa upande wa kushoto wa barabara (madereva wa magari marefu wanaweza kuhitaji kwenda katikati ya barabara ili kuweza kupinda). Kuwa makini na waendesha baiskeli na pikipiki ambao wanaweza kutokea kwa upande wako wa kushoto - waache wakupite na angalia usalama kabla ya kupinda. Kuwa makini na watembea kwa miguu - iwapo kuna watembea kwa miguu wanaovuka barabara upande unaopindia, lazima usimame na kuwaacha wavuke.




KAMWE usilipite gari lingine na kisha kupinda kushoto mbele ya gari hilo.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:32 9/25/08 3:14:50 PM

Kupinda kwenye barabara mbili zinazokwenda upande mmoja. Wakati unavuka au unapinda kulia kwenye barabara mbili za upande mmoja, angalia ili uone iwapo nafasi kati ya barabara hizo mbili (kati) ina upana wa kutosha kumudu urefu wote wa gari lako. Iwapo hivyo ndivyo, pita kwa usalama kwenda katikati na kisha subiri pale hadi upatikane upenyo salama wa magari kwenye barabara ya pili. Iwapo eneo la katikati halina upana wa kutosha, lazima usubiri hadi pale utakapoweza kuzipita njia zote mbili kwa pamoja.

Kupinda kulia kwenye makutano ya barabara mbili wakati gari linalokuja pia linapinda kulia. Utaratibu wa kawaida ni kupinda kulia mbele ya gari jingine (angalia kielelezo hapo chini). Gari jingine linaweza kukuziba kuona magari yanayokuja, hivyo endelea kwa tahadhari na usipinde mpaka uwe na uhakika kuwa njia iko salama.



Fuata ishara ya taa za barabarani. LAZIMA usimame nyuma ya mstari mweupe wa “SIMAMA” isipokuwa kama ishara ni ya kijani. Kama taa za njano zitawaka unaweza kupita iwapo tu umeupita mstari wa simama au uko karibu nao sana kiasi kuwa kusimama kunaweza kusababisha kugongana. Elekea kwenye taa kwa mwendo ambao utakuwezesha kusimama haraka iwapo taa zitabadilika kuwa njano.

Nenda mbele tu wakati taa za kijani zitakapowaka, iwapo njia yako haina vikwazo, au unajiandaa kupinda kulia.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:33 9/25/08 3:14:51 PM

Iwapo taa za barabarani hazifanyi kazi, na hakuna ofisa wa polisi anayeongoza magari, nenda mbele kwa makini, na toa kipaumbele kwa magari yanayotoka kulia kwako.

Kuendesha kwa kujihami. Kwa mfano, wakati unasubiri kupinda kwenda barabara kuu kutoka kwenye barabara za pembeni hakikisha kuwa gari linalotoka kulia na kuashiria kwenda kushoto linaanza kupinda kabla hujaendelea - ikiwa dereva mwingine hana lengo la kupinda kushoto, lakini amesahau kuondoa ishara baada ya kupinda kwa mwanzo.

Ushauri maalumu kwa madereva kwenye sehemu zenye mzunguko

Kabla hujafika kwenye mzunguko hakikisha unapunguza mwendo wako, amua ni njia ipi unahitaji kupitia, angalia kioo chako, na ingia kwenye njia sahihi (angalia ushauri hapo chini) ukifika kwenye mzunguko yaruhusu magari ambayo tayari yako kwenye mzunguko yapite. Angalia kwa makini waendesha baiskeli na pikipiki, ambao inaweza kuwa vigumu kuwaona iwapo kuna magari mengi. Kumbuka kuwa pia kunaweza kuwa na watembea kwa miguu wanaovuka barabara - kutoka kushoto na pia kulia.

Wakati unapinda kushoto:

1. Ashiria kupinda kushoto
2. Pita kwenye njia ya kushoto
3. Yaruhusu magari yaliyo kwenye mzunguko
4. Pita kushoto kwenye mzunguko
5. Endelea sehemu ya kutokea, ukiwa bado umeashiria kushoto.

Wakati unakwenda mbele moja kwa moja:

1. Pita kwenye njia ya kushoto (isipokuwa kama njia ya kushoto imeonyeshwa kwa ajili ya magari yanayopinda kushoto tu) – usionyeshe ishara
2. Ruhusu magari yaliyo kwenye mzunguko yapite
3. Ungana na magari, yaliyo kwenye njia ya kushoto
4. Onyesha ishara ya kwenda kushoto baada ya kupita njia ya kutokea kabla ya ile unayohitaji
5. Endelea kwenye njia yako ya kutokea, ukiwa bado unaonyesha ishara ya kwenda kushoto.


Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:34 9/25/08 3:14:51 PM

Wakati wa kupinda kulia au kupinda kwenye mzunguko:

1. Onyesha ishara ya kwenda kulia
2. Pita kwenye njia ya kulia
3. Yaruhusu magari yaliyo kwenye mzunguko
4. Jiunge na msururu, pita kulia
5. Endelea kuashiria kwenda kulia hadi upite barabara ya kwanza ya kutokea kabla ya ile unayohitaji, kisha onyesha ishara ya kwenda kushoto
6. Endelea kwenda kushoto kwako.

KAMWE usisimame au kuegesha gari kwenye mzunguko**.** Wakati uko kwenye mzunguko usilipite gari refu – linaweza kukugonga kwenye kizingwa.

Njia sahihi ya kuitumia kwenye mzunguko



Uendeshaji wa usiku au kwenye hali mbaya ya hewa

Endesha kwa mwendo ambao utakuruhusu kusimama katika umbali unaouona unafaa. Iwapo utashusha taa zako (yaani kuzifanya zimulike chini), au kumulikwa na ta za magari yanayokuja lazima upunguze mwendo – mbele gizani kunaweza kuwa gari bovu au mwendesha baiskeli.


Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:35 9/25/08 3:14:51 PM

LAZIMA utumie taa usiku (kuanzia nusu saa kabla ya jua kuchwa hadi kuchomoza) au mchana ambapo ni vigumu kuona kwa sababu ya moshi, ukungu, mavunde au mvua kubwa. Kwa mwongozo wa jumla washa taa zako unapokuwa huwezi kuona vizuri kwa zaidi ya mita 100. Usichelewe kuziwasha - zinakufanya uonekane zaidi na wengine.

Angalia taa zako kuwa ni safi, zinafanya kazi na zimerekebishwa vizuri. Taa lazima ziwekwe kiusahihi ili zitoe mwanga wa kawaida bila ya kuwaathiri madereva wengine - fundi wa magari mwenye ujuzi anaweza kukusaidia kuangalia.

Tumia taa zinazomulika chini:

- Wakati magari yanakuja mbele yako
- Wakati unaendesha nyuma ya gari, au unalipita gari jingine
- Wakati unaendesha mijini ambako kuna mwanga wa kutosha mtaani.



Usiwapige mwanga mkali watumiaji wengine wa barabara. Usiwashe taa za mavunde au taa nyingine isipokuwa kama kuna mavunde sana au ukungu.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:36 9/25/08 3:14:53 PM

Kurudi nyuma


USIRUDI nyuma zaidi ya inavyotakiwa.

Kabla ya kurudi nyuma hakikisha kuwa hakuna watembea kwa miguu au vitu kwenye barabara nyuma yako - kumbuka kuwa watoto wadogo wanaweza kuzibwa na sehemu ya nyuma ya gari. Rudi nyuma kwa makini na kamwe isiwe zaidi ya inavyotakiwa. Kama hutaweza kuona vizuri, mtafute mtu akuongoze. Mtu huyu pia anaweza kuwatahadharisha watumiaji wengine wa barabara kupisha. Tumia taa za kukuongoza kurudia nyuma kuwafanya wengine wajue wakati wa mchana, na kuona vizuri wakati wa usiku.

Kuwa makini hasa wakati unarudi nyuma ili utoke kwenye jengo, ua, kiwanja cha nyumbani – kuta au uzio unaweza kuwaziba watembea kwa miguu ambao wanakaribia kupita sehemu ya kutokea gari. Ikiwezekana, geuzia ndani, ili uweze kutoka nje kwa mbele.

Usirudi nyuma kamwe kwenye barabara ndogo pembeni mwa barabara kuu. Usirudi nyuma kamwe kwenye makutano makuu ya barabara. Usirudi nyuma kamwe mahali wavukapo waenda kwa miguu, au mahali reli inapokatisha barabara.

Inashauriwa sana kuwa magari yote ya mizigo mikubwa na magari yote ya kibiashara yawekwe kifaa kinachotoa sauti ambacho kitalia wakati gari linarudi nyuma.



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:37 9/25/08 3:14:54 PM

Kuegesha

Wakati unataka kusimama au kuegesha, kumbuka vioo-ishara-kitendo. Toka nje ya barabara ikiwezekana kwenda kwenye eneo linalofaa kuegesha. Iwapo itakubidi usimame barabarani, simama karibu kadiri iwezekanavyo na upande wa kushoto. Daima angalia iwapo ni salama kuegesha gari na iwapo inaruhusiwa kuegesha mahali hapo. Kabla ya wewe au abiria wako kufungua mlango, hakikisha hutamgonga mtu yeyote anayepita barabarani au kwenye njia ya watembeao kwa miguu – angalia kwa makini waendesha baiskeli na pikipiki. Kumbuka kuwa ni salama kushuka kwenye gari upande wa kushoto karibu na ukingo wa barabara.

USIEGESHE gari:

- bila ya kujali na kuwafikiria wengine
- kwenye alama za pundamilia au mita 5 karibu na alama hizo
- mita 5 ndani ya makutano ya barabara au mahali reli inapokatisha barabara
- kwenye kituo cha basi au mita 15 toka pande zote za alama ya “kituo cha basi”
- kwenye njia ya watembeao kwa miguu
- mbele ya sehemu ya kuingilia magari
- kwenye barabara yenye mistari myeupe miwili ya katikati, hata kama moja ya mistari hiyo umekatikakatika
- ambapo haparuhusiwi kuegesha gari kwenye alama ya HAKUNA kuegesha na/au mistari ya njano kwenye ukingo wa barabara.

Usiegeshe mahali popote ambapo itakuwa hatari au kusababisha matatizo kwa watumiaji wengine wa barabara, kwa mfano:

- karibu na geti la shule
- karibu na kilele cha kilima
- kwenye kona kali
- upande mwingine wa gari lililoegeshwa (uegeshaji wa magari mawili)
- mkabala na kizingwa
- pale ambapo gari lako litakiziba kituo cha teksi
- pale ambapo gari lako litaziba alama au ishara ya barabarani.

Unapoliacha gari lako LAZIMA uhakikishe kuwa haliwezi kutembea. Kamwe usiliache gari bila kuzima injini. Zima injini na taa, na hakikisha breki ya mkono (breki ya kuegeshea) imewekwa. Daima funga gari lako.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:38 9/25/08 3:14:54 PM

Usiegeshe usiku kwenye barabara zenye magari mengi au mahali ambapo magari yanakwenda kwa kasi. Iwapo huwezi kuepuka kufanya hivi, washa taa za kuegeshea. Wakati wa usiku egesha upande wa kushoto wa barabara tu.

Kuwajali watembea kwa miguu na watumiaji wengine wa barabara wanaoweza kuathirika


Kuwa makini na watembea kwa miguu. Watembea kwa miguu wako katika hatari kubwa pindi wanapogongwa na magari. Watembea kwa miguu wengi, hususan wale wa maeneo ya vijijini, hawajazoea barabara zenye magari na hawajui jinsi barabara ilivyo hatari. Endesha kwa makini sana na punguza mwendo hadi km 30 kwa saa au chini ya hapo iwapo kuna watembea kwa miguu mahali hapo, hususan katikati ya miji yenye watu wengi, kwenye masoko na karibu na vituo vya mabasi. Kuwa makini na watembea kwa miguu wanaovuka barabara ghafla kutoka nyuma ya gari lililoegeshwa au kusimama (labda basi).



Kuwa makini sana kama watoto wako karibu, na wakati unaendesha karibu na shule. Usiwategemee watoto kutenda kama watu wazima. Uwezo wao wa kuona na kusikia una ukomo zaidi, na hawawezi kutambua mwendo vizuri. Hawako makini, na wanapokuwa hatarini wanaweza kusimama wametulia kwa hofu, badala ya kuondoka mahali hapo. Mahali ambapo pana watoto punguza mwendo na kuwa makini sana.


Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:39 9/25/08 3:14:55 PM

Wasaidie wazee na walemavupindi inapokuwa vigumu kwao kuvuka barabara. Waache wavuke kama ni salama kufanya hivyo. Daima punguza mwendo unapokuwa karibu na shule na hospitali.



Iwapo kuna watembea kwa miguu wanaovuka barabara mahali ambapo unapinda kuelekea huko, simama na kuwaacha wavuke mbele yako.

Alama za Pundamilia. Unapofika kwenye mahali pa kuvukia watembea kwa miguu penye alama za mistari myeupe ("alama za pundamilia") uwe tayari kupunguza mwendo na kusimama kuwaacha watu wapite. LAZIMA usimame kama mtu yeyote anavuka au anakaribia kuvuka. USILIPITE gari lolote ambalo limesimama kuruhusu watembea kwa miguu kuvuka. Na USIEGESHE gari lako kwenye kivuko cha watembea kwa miguu – au ndani ya eneo la umbali wa mita 5 karibu yake.



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:40 9/25/08 3:14:55 PM

Ishara zinazoongoza kuvuka kwa watembea kwa miguu. Sehemu nyingine za kuvukia zinaongozwa na taa za barabarani. Fuata ishara za taa za barabarani. Watembea kwa miguu wanaweza kuvuka barabara mbele yako kukiwa na taa NYEKUNDU.

Kuwa makini na waendesha pikipiki na baiskeli. Vyombo vyenye magurudumu mawili ni vigumu zaidi kusimama ukilinganisha na magari makubwa. Daima viangalie vyombo hivyo unapoingia na kutoka kwenye makutano. Wape waendesha pikipiki na baiskeli nafasi ya kutosha wakati unawapita, hususan iwapo unaendesha gari refu au gari linalovuta tela. Kamwe usiwapite na kupinda karibu mbele yao. Wachukulie waendesha mikokoteni kwa uangalifu uleule.

Misululu. USIENDESHE kuupita msululu, mstari wa watoto wa shule, au kundi.

Usizuie magari ya dharura au magari ya msafara wa viongozi. Madereva wa magari ya dharura yaliyoruhusiwa wanaweza wasifuate sheria za barabarani wakati wa dharura ilimradi watumie kimulimuli au king'ora cha tahadhari, na wasiendeshe kwa hatari. Madereva wengine LAZIMA wayapishe magari hayo ya dharura. USIZUIE msafara wa viongozi. Ukiuona unakuja, nenda kwenye ukingo wa kushoto wa barabara na simama mpaka upite. Fuata maelekezo ya maofisa wa polisi na watu wa kwenye magari yanaousindikiza.

Panapokatisha Reli

Reli inayokatisha bila vizuizi, ishara au mtu yeyote anayeongoza magari, punguza mwendo kabla ya kuingia kwenye reli ili kuchunguza kama magarimoshi yanakuja. Madereva wa mabasi, na magari yanayobeba vitu vinavyoweza kuwaka moto, LAZIMA wasimame na kuangalia kabla ya kuendelea. Sikiliza king'ora cha garimoshi. Kamwe usishindane na magarimoshi – mara zote yana haki ya kupita kwanza. Hakikisha ni salama kabla ya kuvuka, na uwe makini zaidi pale penye njia za reli zaidi ya moja.

Pale ambapo reli inayokatisha inaongozwa na vizuizi, ishara au mtu mwenye mamlaka hayo, LAZIMA uvifuate. Kamwe usijaribu kuongeza mwendo ili upite haraka wakati vizuizi vinashushwa chini. Kamwe usiondoke hadi alama za taa zinapozima na vizuizi vimefunguliwa kabisa. Waache watembea kwa miguu na waendesha baiskeli wapite kwanza.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:41 9/25/08 3:14:56 PM

Kamwe usiendeshe kwenye reli mpaka njia iwe imeruhusiwa upande linakopita na usikaribie gari lililoko mbele yako. Kamwe usiegeshe au kusimama karibu na reli. Iwapo gari lako litaharibika kwenye reli, watu watoke ndani ya gari haraka na kukaa mbali na hatari. Mwarifu msimamizi wa reli, kama yupo, na fuata maelekezo yake. Vinginevyo, piga simu polisi. Iwapo hakuna garimoshi linalokuja omba msaada wa kulisukuma gari kutoka kwenye reli. Iwapo utalisikia au kuliona garimoshi likija ondoka kwenye reli haraka, na jaribu na kumwashiria dereva wa garimoshi bila ya kujiweka hatarini.

Usijitie hatarini kwenye reli inayokatisha barabara. Iwapo utagongana na garimoshi ni vigumu kupona.

Ajali za Barabarani za Kawaida



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:42 9/25/08 3:14:56 PM

Kuharibika

Iwapo gari lako litaharibika, au kupata pancha, jaribu na lisogeze gari lako nje ya barabara. Kama hili haliwezekani liweke gari karibu na ukingo wa kushoto wa barabara na mbali ya makutano, madaraja na kona na sehemu nyingine za hatari.

Iwapo huwezi kuepuka kusimama barabarani LAZIMA utoe tahadhari kwa magari mengine kwa kuweka kiashiria chekundu cha pembetatu karibu na ukingo wa barabara si chini ya umbali wa m30 nyuma ya gari - pamoja na kiashiria kingine cha pembetatu katika umbali uleule mbele ya gari. Pia lazima utumie taa zako za tahadhari ya hatari (indiketa mbili - zote zikiwaka kwa pamoja). Iwapo umesimama kwenye kona au karibu ya kilele cha kilima mtu moja arudi nyuma barabarani kuyatahadharisha magari yanayokuja.



LAZIMA ujaribu na kuliondoa gari haraka iwezekanavyo. Ofisa wa polisi ana mamlaka ya kupanga namna ya kuliondoa gari lolote iwapo ataona linahatarisha usalama. Utapaswa kulipa gharama za kuliondoa.

Jaribu kutosimama au kutoshughulika na gari mahali ambapo utakuwa katika hatari ya kugongwa na magari yanayopita. Unapolitengeneza gari usimwage dizeli au mafuta mengine barabarani, kwani yanaweza kuiathiri barabara.

Fanya kila jitihada kulitengeneza gari au kuliondoa barabarani. Kabla ya giza kuingia. Iwapo utalazimika kuliacha gari bovu barabarani usiku, washa taa za kuegeshea na hakikisha kuwa kuna vibao vya tahadhari vya pembetatu vilivyowekwa umbali unaofaa barabarani kabla ya gari kuwatahadharisha madereva wengine. Waarifu Polisi.

Hakikisha kuwa mawe uliyotumia kuzuia matairi ya gari yameondolewa barabarani wakati unapoondoka.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:43 9/25/08 3:14:57 PM

Iwapo kuna ajali

Iwapo umehusika kwenye ajali au umesimama kusaidia:

- wape tahadhari madereva wa magari mengine kwa kuwasha taa zako za tahadhari ya hatari (indiketa mbili) na, ikibidi, waashirie madereva wengine wapunguze mwendo-dhibiti magari ili kuepuka ajali nyingine – waombe madereva wengine na wanakijiji wakusaidie kufanya hivi
- waombe madereva kuzima injini zao na sigara zozote
- wasiliana na Polisi mara moja – waeleze eneo hasa la ajali na idadi ya magari na idadi ya watu waliojeruhiwa – waombe watu wengine kufanya hivi ili kuhakikisha kuwa ujumbe umefika.
- Jiandae kutoa huduma ya kwanza – iwapo majeruhi wameumia sana, na kuna matumaini madogo ya kupata msaada haraka, fanya utaratibu wa kuwapeleka majeruhi kwenye hospitali ya karibu
- Wahudumie walioathirika na mali zao – na mshawishi kila mmoja kufanya hivyo.
- Usichukue sheria mikononi mwako – usiruhusu watu wampige aliyesababisha ajali.

Ukiyaona magari yamesimama mbele, punguza mwendo na uwe tayari kusimama. Iwapo ukiona tayari kuna watu wa kutosha wanaotoa msaada usisimame na kusababisha msongamano. Wakati unapita mahali penye ajali usibabaike – kuwa makini na barabara mbele yako. Fuata amri za maofisa wa Polisi walio kwenye tukio, na kuwa mvumilivu iwapo kutakuwa na kukaa kwa muda mrefu.

Iwapo umehusika kwenye ajali na mtu amejeruhiwa LAZIMA utoe jina na anwani yako (na jina na anwani ya mmiliki wa gari, kama ni tofauti) kwa mtu yeyote aliyehusika na LAZIMA utoe taarifa ya ajali kwenye kituo cha polisi cha karibu au kwa ofisa wa polisi haraka iwezekanavyo (na kamwe isiwe zaidi ya saa 12 baada ya ajali. Taarifa itawasaidia Polisi, waendesha mashtaka, na Kampuni za Bima kubainisha kilichotokea na iwapo kuna mwenye kosa ambaye anatakiwa kufidia gharama.

LAZIMA usimame na kuwasaidia watu waliojeruhiwa kwenye ajali, isipokuwa kama unahofia usalama wako. Iwapo umehusika kwenye ajali ya barabarani ambapo hakuna aliyejeruhiwa huhitaji kutoa taarifa Polisi, lakini LAZIMA utoe jina na anwani yako (na jina na anwani ya mmiliki wa gari, kama ni tofauti) na namba ya usajili ya gari lako kwa mtu mwingine yeyote aliyehusika.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:44 9/25/08 3:14:58 PM

Huduma ya Kwanza

Waathirika wengi wa ajali za barabarani hutaabika bila sababu, au hata kufa, kwenye eneo la ajali kwa sababu ya kukosekana kwa uangalizi wa kutosha. Mtu mwenye mafunzo ya Huduma ya Kwanza daima anaweza kuzuia hali ya mtu aliyejeruhiwa kuwa mbaya na anaweza kuokoa maisha yao. Madhumuni ya Huduma ya kwanza ni:

1. Kuokoa maisha
2. Kukinga majeruhi au ugonjwa kuzidi kuwa mbaya
3. Kuleta nafuu

Mafunzo ya Huduma ya Kwanza yako kwenye vituo vingi na kwenye asasi mfano Chama cha Msalaba Mwekundu, na ni jambo la busara kujifunza maarifa haya. **Lakini hata kama huna mafunzo ya Huduma ya Kwanza kuna baadhi ya vitu vyepesi unavyoweza kufanya kuwasaidia majeruhi,** na hivi vimeelezwa hapo chini kwa kufuatisha kipaumbele.

1. Zuia madhara zaidi na kuwa salama zaidi

Kwanza kabisa chunguza madhara yako, majeruhi na wengine. Weka mazingira salama kabla ya kuwahudumia. Chukua tahadhari usijeruhiwe. Kwa mfano, toa tahadhari na dhibiti magari yanayokuja kuzuia ajali nyingine. Waombe watu wengine wakusaidie katika jambo hili. Iwapo kuna hatari ya moto, hakikisha hakuna mtu anayevuta sigara au kutumia kiberiti.

2. Matibabu ya dharura

Kitu cha muhimu zaidi ni kuokoa maisha. Kumbuka **"Dkt A.B.C. "** Hii inasimama kwa:

D = Danger (Hatari) kuna madhara yanayoendelea kwa majeruhi? – Jaribu kuleta usalama. Watenganishe majeruhi na wale unaodhani hawajajeruhiwa sana.

R = Response (Mwitikio) Kuna mwitikio wowote kutoka kwa majeruhi? – Angalia hali ya sauti inavyotoka au mguso. Iwapo hakuna mwitikio chunguza njia ya hewa (koo).




A = Airway (Njia ya hewa) Je, njia ya hewa (koo) haina kikwazo? Mlaze majeruhi chali, Inua kichwa upande mmoja , halafu fungua mdomo, angalia kuwa ulimi hauzibi koo na tumia vidole vyako kutoa chochote kilichopo mdomoni (chakula, uchafu, meno bandia n.k.)

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:45 9/25/08 3:14:58 PM

na taratibu sogeza kichwa ili kidevu kiwe juu na mdomo ufungukei, kisha angalia upumuaji.

B = Breathing (Upumuaji) Je, majeruhi anapumua? – chunguza kwa kuweka sikio lako karibu na mdomo wa majeruhi kwa angalau sekunde 10 kusikiliza na kuhisi pumzi. Angalia kama kifua kinainuka na kushuka. Iwapo hakuna pumzi, haraka haraka mpulizie pumzi kwa kubana pua, mpumulie pumzi zaidi majeruhi mpaka utakapomalizia pumzi yako kwenye mapafu yake Endelea kufanya hivyo. Angalia tena upumuaji. Iwapo bado hapumui, angalia mzunguko wa damu.



C = Circulation (Mzunguko wa Damu) Je, kuna mapigo ya moyo? – Angalia mapigo ya moyo kwa kuweka vidole viwili shingoni, na angalia rangi ya macho na mboni za majeruhi. Iwapo hakuna kupumua au mzunguko wa damu, tafuta msaada wa dharura haraka kabla ya kuendelea. Pindi msaada utakapokuwa umetafutwa, iwapo unajua utaalamu huu, kisha tumia CPR (Cardio – Pulmonary Resuscitation – Uchocheaji mapafu) ambayo huhusisha ubanaji kifua na upumuaji bandia hadi msaada wa mtaalam utakapofika, au majeruhi atakapoanza kupumua.

Kama kuna mapigo ya moyo lakini majeruhi hajapumua, endelea kumpumulia pumzi (pumzi kila baada ya sekunde tano). Usikate tamaa – inaweza kuchukua muda kuweza kupumua yeye mwenyewe.

Majeruhi atakapoweza kupumua na kuongea tena, mlaze chali na mtie joto. Iwapo anapumua lakini hawezi kujibu maswali, muweke sehemu salama ya kupumzikia (angalia Sehemu ya 7).

3. Pata msaada

Msaada wa mtaalam lazima uitwe haraka iwezekanavyo, kwa kawaida kwa kupiga simu 112. Usijaribu kumuacha majeruhi peke yake, hivyo ikiwezekana waombe wengine kupiga simu au kutafuta msaada na wakuarifu kuwa wamefanya hivyo. Siku hizi watu wengi wana simu za mkononi kwa hiyo kunaweza kusiwe na sababu ya kuondoka mahali pa

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:46 9/25/08 3:14:59 PM

tukio. Ni muhimu kutoa huduma sahihi za dharura za taarifa ya:

- Eneo la ajali – jina la mtaa, alama kuu inayojulikana au mahali
- Aina ya ajali
- Hali ya mazingira na hatari zilizopo
- Idadi ya watu waliojeruhiwa na ukubwa wa majeruhi.

Usikate simu kwanza - subiri mhusika na msaada wa dharura kuthibitisha kuwa ameielewa taarifa yako.

Kama msaada haupatikani karibu itakubidi kumsafirisha majeruhi kwenye sehemu ya huduma ya matibabu. Tafuta ushauri wa Polisi na wenyeji na kuwauliza sehemu nzuri ya kumpeleka majeruhi. Huduma ndogo kama ya vituo vya afya na kliniki vinaweza kuwa msaada kwa hali ya majeruhi aliyeumia vibaya, ili kuwepo na uwezekano wa kufika hospitali baada ya safari ndefu. Ingawa baadhi ya hospitali huenda zisiwe wazi kwa masaa 24.

4. Kuwaondoa majeruhi

Usimuondoe majeruhi yeyote isipokuwa kama ni lazima sana. Majeruhi walio kwenye gari bado wasiotolewe isipokuwa kama kuna hatari ya haraka ya moto, kudhurika zaidi, au ajali zaidi. Majeruhi wa kuvunjika mifupa au wa uwezekano wa majeraha ya ndani au uti wa mgongo wasiondolewe isipokuwa kama ni muhimu kwa usalama wao. Iwapo majeruhi hawana fahamu lakini wanapumua na hawaonekani dhahiri kuumia vibaya, waweke kwenye mahali pa kupata nafuu (angalia chini) kuzuia matatizo ya upumuaji.

5. Tiba ya uvujaji damu na majeraha



Mtu anaweza kuvuja damu hadi kufa katika muda wa dakika tano, hivyo ni muhimu kujaribu na kuzuia upotevu wa damu nyingi. Ikiwezekana, mlaze sehemu iliyonyooka. Tafuta damu inakotokea. Halafu angalia kama kuna chochote kwenye jeraha na kiondoe kama ni rahisi kufanya hivyo. Iwapo kuna kitu ndani ya jeraha kiache, na tumia msukumo wa hewa karibu na kidonda.

Kifunge jeraha vizuri kwa kubana, hasa ukitumia kitambaa chenye dawa kutoka kwenye Kisanduku cha Huduma ya Kwanza au kitu kingine safi – vinginevyo tumia mikono yako (Unapokuwa unashughulikia jeraha kinachovuja damu cha mtu mwingine, inapendekezwa kuwa ujilinde

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:47 9/25/08 3:15:01 PM

mwenyewe kwa kuvaa glovu au mifuko ya plastiki iliyosafi). Iwapo damu haipungui kutoka, bana zaidi. Utaweza kufunga zaidi jeraha, lakini kuwa makini usije ukazuia mzunguko wa damu – fungua kidogo kidogo kila baada ya dakika kumi ili kupunguza mgandamizo. Iwapo hakuna mifupa iliyovunjika, inua juu kiungo kinachovuja kupunguza mtiririko wa damu.

6. Wahudumie waathirika wa mshituko

Pia ni muhimu sana kutambua, kuzuia na kutibu dalili za mshituko, kwani huu unaweza kuleta madhara makubwa zaidi kuliko jeraha la awali. Dalili ni: baridi, kusawajika, kufifia kwa ngozi, upumuaji wa haraka au wa taratibu, homa; kupiga miayo au kushusha pumzi.


Sababu za mishituko ni nyingi, ikiwa ni pamoja na: majeraha; kushuka kwa shinikizo la damu; na kupungua kwa kiwango cha majimaji yoyote ya mwili. Pamoja na kushughulikia sababu, ni muhimu kutomuacha majeruhi peke yake, na kuwawekea mazingira mazuri zaidi kwa:

1. kumlaza chini majeruhi
2. kumlegeza nguo yoyote inayombana hususan kuzunguka kifua na kwenye njia za hewa
3. kumpatia joto majeruhi kwa kumfunika kwa blanketi
4. kuzungumza na majeruhi kuwafanya wawe watulivu
5. kunyosha miguu kidogo ili kuifanya damu iendelee kwenda kichwani.

Majeruhi wa ajali kamwe asipewe kitu chochote kula au kunywa. Iwapo wana kiu, rowesha midomo yao kwa maji. Kamwe usimpe majeruhi dawa yoyote au kutumia kitu chochote isipokuwa maji safi na kufunga bendeji majeruhi.

7. Mweke majeruhi katika mazingira mazuri ya kupona

Haya ni mazingira mazuri kwa majeruhi kulala kiubavu, huzuia kukabwa na ndimi zao au kuzuia kutapika kama hawana fahamu. Kichwa kirudishwe nyuma kidogo, mkono wa chini uwe nje kwenye pembe sahihi (nyuzi 90), mkono wa juu uwe chini ya shavu, mguu wa chini unyooshwe nje, na mguu wa juu upinde katika pembe sahihi kama inavyoonyeshwa kwenye mfano wa chini.



Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:48 9/25/08 3:15:01 PM

Alama za barabarani


Alama za barabarani zinasaidia kutoa tahadhari, kurekebisha, kuongoza na kuwapa taarifa watumiaji wa barabara. Zinajumuisha ishara za barabarani kwenye nguzo za wima, taa za barabarani, na michoro ya barabarani.

Kuna makundi manne ya alama za barabarani:

Alama za udhibiti	kuwaambia madereva kipi wafanye na kipi wasifanye
Alama za tahadhari	kuwatahadharisha madereva juu ya hatari au matatizo ya barabara mbele
Alama za taarifa	kuwasaidia madereva kuangalia huduma na maeneo wanayoyataka
Alama za mwongozo	kuwasaidia madereva kuona njia za wanakokwenda

Alama za makundi mengine zina umbo maalum na rangi kuwasaidia madereva kuzitambua haraka. Alama mbili muhimu sana alama za “Simama” na “Ruhusu,” zina maumbo yake maalum.

Kama pana haja ya kupambanua au kupanua taarifa ya kwenye alama kuu taarifa ya ziada imejumuishwa kwenye bamba chini ya alama kuu.



Ishara za barabarani zinatumika kudhibiti magari na watembea kwa miguu kwenye makutano na kwenye alama za pundamilia.

Michoro ya barabarani inagawanywa kwenye michoro ya udhibiti, tahadhari na mwongozo.

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:49 9/25/08 3:15:02 PM

Alama za Kudhibiti



R1
Simama




R.1.5
Kizuizi cha simama / nenda



R2
Ruhusu



R3
Hakuna kuingia



R4
Kuna njia moja (kushoto, kulia, moja kwa moja)



R6
Ruhusu magari yanayokuja mbele yako



R103
Pita kushoto



R104
Pita kulia



R105
Endelea kushoto tu



R106
Endelea kulia tu



R107
Endelea moja kwa moja tu



R108
Mbele pinda kushoto



R109
Mbele pita kulia



R110
Njia ya watembea kwa miguu



R111
Njia ya waendesha baiskeli tu



R121
Basi peke yake



R137
Mzunguko



R201
Ukomo wa mwendo



R202
Hairuhusiwi kupita magari yenye zaidi ya t12



R203
Hairuhusiwi kupita magari yenye zaidi ya ekseli ya t2

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:50 9/25/08 3:15:02 PM

Alama za Kudhibiti (zinaendelea)



R204
Hairuhusiwi kupita magari yenye kimo zaidi ya m4.4



R205
Hairuhusiwi kupita magari yenye urefu zaidi m15



R206
Hairuhusiwi kupiga honi



R209
Mbele usipite kushoto



R210
Mbele usipite kulia



R211
Usipite kushoto



R212
Usipite kulia



R213
Hairuhusiwi kugeuza kurudi ulikotoka upande wa pili



R214
Usilipite gari mbele yako



R216
Hairuhusiwi kuegesha magari



R217
Hairuhusiwi kusimama



R218
Watembea kwa miguu hawaruhusiwi kupita hapa



R219 Waendesha baiskeli hawaruhusiwi kupita hapa



R220 Waendesha baiskeli na watembea kwa miguu hawaruhusiwi kupita hapa



R222
Waendesha pikipiki hawaruhusiwi kupita hapa



R223
Magari madogo hayaruhusiwi kupita hapa



R224
Teksi haziruhusiwi kupita hapa



R225
Mabasi madogo hayaruhusiwi kupita hapa



R227
Mabasi hayaruhusiwi kupita hapa



R229
Mabasi ya mizigo hayaruhusiwi kupita hapa

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:51 9/25/08 3:15:02 PM

a

01
ec
a a
sin

A
Z

Alama za Tahadhari



W102
Barabara inakatisha katika barabara muhimu



W104
Makutano-T



W105
Makutano T-mshazari (kulia)



W106
Makutano T-mshazari (kushoto)



W107
Makutano ya barabara upande



W108
Makutano ya barabara upande wa (kulia)



W109
Makutano tofauti (kulia - kushoto)



W110
Makutano tofauti (kushoto - kulia)



W111
Makutano makali (nusu kushoto)



W112
Makutano makali (kushoto)



W113
Makutano makali (nusu kulia)



W114
Makutano makali (kulia)



W115
Makutano-Y



W116 Mwisho wa udhibiti wa matumizi ya sehemu ya barabara mbili (kulia)



W117 Mwisho wa udhibiti wa matumizi ya sehemu ya barabara mbili (moja kwa moja)



W118 Mwanzo wa udhibiti wa matumizi ya sehemu ya barabara mbili (moja kwa moja)



W119 Mwanzo wa udhibiti wa matumizi ya sehemu ya barabara mbili (kushoto)



W201
Mzunguko



W202 Barabara imepinda (kulia) kwenye mteremko usio mkali



W203 Barabara imepinda (kushoto) kwenye mteremko usio mkali

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:53 9/25/08 3:15:03 PM

Alama za Tahadhari (zinaendelea)



W204
Kona kali (kulia)



W205
Kona kali (kushoto)



W206
Kona kali kwenye mwinuko (kulia)



W207
Kona kali kwenye mwinuko (kushoto)



W208
Barabara imepinda (kulia-kushoto)



W209
Barabara imepinda (kushoto-kulia)



W210
Kona mbili kali zimeungana (kulia-kushoto)



W211
Kona mbili kali zimeungana (kushoto-kulia)



W212
Barabara ya njia mbili




W213
Barabara ya njia mbili inakatisha



W301
Mbele kuna taa za kuongoza magari



W302
Mbele simama kuna kizuizi cha magari



W303
Mbele kuna kizuizi cha magari "Toa njia"



W306
Kivuko cha watembea kwa miguu



W307
Njia ya watembea kwa miguu



W308
Kivuko cha watoto



W309
Kivuko cha waendesha baiskeli



W310
Kivuko cha mifugo



W313
Hifadhi ya wanyamapori



W318
Reli inakatisha

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:54 9/25/08 3:15:04 PM

Alama za Tahadhari (zinaendelea)



W319
Barabara inapita chini ya mlima



W320
Hairuhusiwi kupita magari yenye kimo zaidi ya m4.4



W321
Hairuhusiwi kupita magari yenye urefu wa zaidi ya m15



W322
Mteremko mkali



W323
Mwinuko mkali



W326
Daraja jembamba



W327 Hairuhusiwi kupita magari yenye zaidi ya upana unaokubalika



W328
Barabara nyembamba pande zote



W329
Barabara nyembamba kutoka upande wa kulia



W330
Barabara nyembamba kutoka upande wa kushoto



W331
Barabara ina matuta



W332
Matuta ya kupunguza mwendo



W333
Barabara inateleza



W334
Maporomoko ya mawe (kutoka kulia)



W335
Maporomoko ya mawe (kutoka kushoto)



TW336
Ujenzi unaendelea



TW338
Kuna changarawe zisizoshindiliwa



W339
Tahadhari kwa ujumla



TW340
Barabara iliyopungua unene



TW343 Mbele kuna kizuizi cha "Simama / Nenda"

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:55 9/25/08 3:15:04 PM



W349
Upepo uvumao
uelekeo wa safari



W350
Mkond
s



dege
hini



barabarani

magari

Alama za Taarifa



IN4 Barabara isiyotoka mbele



IN5 Barabara isiyotoka kulia



IN6 Barabara isiyotoka kushoto

Alama za ujumbe wa pili



IN11
Taarifa ya alama kuu inayotumika kwenye mwelekeo huu (mfano)



IN11
Taarifa ya alama kuu inayotumika katika aina hii ya gari (mfano)



IN12 Taarifa ya alama kuu inayotumika kwenye mwelekeo huu (mfano)



IN16 Mbele kuna kituo cha basi km1



IN20 Toa njia kwa magari yanayokuja mbele yako



IN11
Alama ya ziada (mifano)


Alama za kuongoza



GD1
Alama ya mwelekeo (kabla ya makutano)



GD1
Alama ya mwelekeo (kabla ya makutano) na jina la mtaa mmoja



GD8
Alama ya mwelekeo (kabla ya mzunguko)



GD2
Alama ya mwelekeo (kwenye makutano)




GD2
Alama ya mwelekeo (kwenye makutano) na kambi ya utalii



GD4 Alama inayoonyesha mji mdogo



GF3 Alama ya mwisho wa kupinda-kituo cha utali



GD3
Alama za kufuata (baada ya makutano)



GDL2
Alama ya mwelekeo (kwenye makutano) barabara za maeneo



Mafuta/gereji Maliwato Mgahawa



Hospitali Huduma ya kwanza Polisi

GFS Huduma vivutio (mfano)

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:57 9/25/08 3:15:05 PM

Alama za kuongoza (zinaendelea)




GL3
Jina la mji




GL4
Jina la mto



GS101
Mwisho wa njia ya kushoto




GS205
Njia imeongezwa upande wa kushoto




GS805
Alama ya njia ya kuchagua mwanzoni (mfano)

Taa za kuongoza magari



S1 - Ishara za kawaida
"Nyekundu ni kuwa LAZIMA usimame, kijani ni kuwa unaweza kwenda moja kwa mbele, au unaweza kupinda kushoto au kulia kama njia haina vikwazo, njano maana yake LAZIMA usimame, isipokuwa kama umekaribia mstari wa kusimama ambapo huwezi kusimama kiusalama"




S2-S7
Mshale wa kijani inamaanisha kuwa "unaweza kuendelea tu kwenye mwelekeo ulioonyeshwa na mshale"



S1H
Wakati ishara zinaonyesha mbele zinaweza kuonyesha pia pembeni kama inavyoonyeshwa na mifano hii miwili



S11 - Alama za watembea kwa miguu
Nyekundu maana yake ni kuwa usipite, kijani maana yake pita kwa uangalifu, mtu mwekundu inayowaka na kuzima maana yake usianze kuvuka



FRD Alama za reli kukatisha Ikiwaka nyekundu "LAZIMA usimame"

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:58 9/25/08 3:15:07 PM

Michoro ya Barabarani

Michoro ya Kudhibiti (LAZIMA uifuate michoro hii)



RTM1
Mstari wa kusimama

RM1
Usiyapite magari mengine

RM5.1
Kitenga njia inayoendelea (usiendeshe kwenye mchoro isipokuwa kama kuna dharu

RM6
Eneo la kuegesha magari

RM9.1
Njia ya basi

RM10 Makutano ya kisanduku (usiingie kwenye kisanduku isipokuwa kama kutoka kwako ni salama)

RM11 Eneo la zigizaga Mstari karibu na kivuko cha pundamilia (usisimame isipokuwa wakati unaruhusu wa enda kwa miguu kuvuka)

RM13
Hakuna kuegesha (wakati wote)

RM13
Hakuna kuegesha (muda maalumu)

RM15 Mchoro wa mzunguku (yaruhusu magari ya kutoka kulia)

Michoro ya Barabarani (zinaendelea)

Michoro ya Tahadhari



WM1
Reli inakatisha mbele



WM2 Mstari unaoendelea - kati ya barabara na barabara nyingine sehemu ya kando ya makutano




WM3
Mstari unaogawanya - kati ya magari yanayokwenda katika maeneo tofauti



WM5
Toa njia mbele kuna kizuizi




WM6
Mshale wa punguzo la barabara (mfano)




WM7
Mshale wa kuonyesha eneo la barabara (mifano)




WM8.1
Mbele hakuna mstari wa kuyapita magari ya njia



WM10
Tuta la kupunguza mwendo



WM12
Matuta madogo ya kupunguza mwendo



WM11.1
Mwisho wa matumizi maalumu ya njia ya basi


Michoro ya Kuongoza



GM1 Mchoro wa mstari wa kutenganisha barabara



GM2.1
Mchoro wa mstari wa mwongozo wa kona



GM2.2
Mchoro wa mstari wa kuongoza watembea kwa miguu



GM3
Mchoro wa mshale wa kuonyesha njia inapanda (mfano)



GM6.1
Eneo la baiskeli



GM7
Alama ya neno (mfano)



GM8
Mchoro ya tahadhari ya ukingo



GM9 Mchoro wa kupunguza mwendo (mfano)

Highway Code-Inside-Swa.indd Sec1:60 9/25/08 3:15:08 PM